# UYUI YA SAMIA




**Jarida Toleo**
**Na. 1**

# UYUI LANGO KUU LA MKOA WA TABORA





JENGO LA UTAWALA HALMAASHAURI WILAYA YA UYUI




JENGO LA UTAWALA HALMASHAURI YA WILAYA YA UYUI




UKUMBI WA MIKUTANO HALMASHAURI YA WILAYA YA UYUI

Wilaya ya Uyui ni miongoni mwa Wilaya saba (7) za Mkoa wa Tabora. Wilaya hii inapakana na Wilaya za Igunga na Nzega kwa upande wa Kaskazini, Wilaya ya Sikonge kwa upande wa kusini, Wilaya ya Kaliua na Urambo kwa upande wa Magharibi, wakati mkoa wa Singida uko upande wa mashariki mwa Wilaya. Katika suala la utambuzi wa kimataifa, Wilaya iko kati ya $05^0 45'$ na $06^0 55'$ kusini mwa ikweta na kati ya $32^0 85'$na $34^0 15'$ mashariki mwa Griniwichi.

Wilaya ina jumla ya kilometa za mraba zipatazo 11, 806. Eneo linalofaa kwa kilimo ni Km2 4,709 lakini eneo linalolimwa ni km$^2$ 1,500 (He 150,000) sawa na asilimia 31.8 ya eneo lote linalofaa kwa kilimo.

Wilaya ina eneo la misitu na hifadhi lenye ukubwa wa km$^2$ 2,217**.** Aidha, lipo Eneo la misitu ya kawaida (isiyokuwa ya hifadhi) lenye ukubwa wa km$^2$ 3,837**.** Lipo pia eneo la mbuga linalotumika kwa malisho km$^2$ 2,690.

Wilaya ya Uyui iimeundwa na Halmashauri 1, Tarafa 3 ambazo ni Ilolangulu, Uyui na Igalula, Kata 30, Vijiji 156, vitongoji 706, Majimbo 2 ya Uchaguzi (Jimbo la Uyui na Jimbo la Igalula). Kwa Mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya waka 2012 Wilaya ya Uyui ilikuwa na jumla ya wakazi 396,623, Kulingana na Sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022, idadi ya wakazi wa wilaya ya Uyui imeongezeka na kufikia 562,588 (wanaume 276,261 na wanawake 286,327) kukiwa na ongezeko la watu 165,261.



**BAADHI YA MAJENGO KATIKA HOSPITALI YA WILAYA YA UYUI**



**JENGO LA UTAWALA SHULE YA SEKONDARI NTAHONDI KATA YA ISILA**

Kwa upande wa Sekta ya Elimu Sekondari kiasi cha **shilingi 13,555,645,710** kimetumika kutekeleza miradi ikiwa ni pamoja na ongezeko la shule kutoka **27** hadi **34** zikiwemo shule mpya **7**, kidato cha tano na sita kutoka shule **2** hadi shule **5**, vyumba vya madarasa **260** vimejengwa na maabara **41** zimejengwa na idadi ya wanafunzi (udahili) imeongezeka kutoka **12,049** hadi **17,446.**

Ujenzi wa shule ya sekondari Ntahondi katika Kata ya Isila Wilaya ya Uyui imesaidia upatikanaji wa elimu kwa wanafunzi waliokuwa wakitembea umbali wa km 6 kwenda shule hiyo, kwa sasa wanatembea umbali wa km 1.

Shule hii ilianza ujenzi wa madarasa matatu mwaka 2021 ambapo ilianza na nguvu za wananchi pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Uyui, baada ya uongozi wa awamu ya sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan ujenzi huo uliendelea kwa kuongeza madarasa pamoja na mabweni ya wasichana na wavulana.

Mkuu wa shule hiyo ndugu Stephano Manga amesema kabla ya ujenzi huo wa Sekondari wanafunzi walikuwa wakitembea umbali wa Km 6 lakini kwa sasa wanatembea umbali wa km 1 na kupelekea ongezeko la ufaulu kwa wanafunzi.

Aidha ndugu Manga amesema kuwa katika ujenzi wa sekondari hiyo pia wanafunzi wamejengewa mabweni ya wasichana na wavulana hii inasababisha kupunguza utoro shuleni. Pia katika ujenzi huo, Manga amesema nyumba mbili za walimu za sehemu moja zimejengwa hii inapelekea kupunguza ukosefu wa nyumba za walimu ili wanapofanya kazi wafanye kwa weledi.




Upande wa Sekta ya Elimu Msingi, kiasi cha shilingi **8,582,719,496.00** kimetumika katika Sekta hii na kupelekea ongezko la idadi ya shule kutoka **154** hadi **182,** ujenzi wa vyumba **70** vya madarasa na matundu **112** ya vyoo na kupunguza msongamano na kuongezeka kwa ufaulu wa darasa la saba kutoka asilimia **54.0** hadi **58.1.**



**BAADHI YA MABWENI YA WAVULANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI NTAHONDI**



**BAADHI YA MABWENI YA WASICHANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI NTAHONDI**





NYUMBA MBILI ZA WALIMU KATIKA JENGO MOJA



MATUNDU YA VYOO KATIKA SHULE YA SEKONDARI NTAHONDI KATA ISILA WILAYA YA UYUI




JENGO LA UTAWALA SHULE YA MSINGI KADAMA




JENGO LA SHULE AWALI KADAMA



MAJENGO YA SHULE YA MSINGI MIGUSA KATIKA KIJIJI CHA MIYENZE KATA YA MIYENZE




MAJENGO YA MADARASA SHULE YA MSINGI MIGUSA



MAJENGO YA MADARASA YA SHULE YA MSINGI MIGUSA




MADARASA YA SHULE YA AWALI



Halmashauri ya Wilaya ya Uyui imefanikiwa kutoa mikopo yyenye thamani ya **shilingi 1,703,114,470** kwa vikundi **395** ambapo vikundi **229** vya Wanawake vimekopeshwa kiasi cha **shilingi 1,011,000**, vikundi vya Vijana **116** kiasi cha **shilingi 570,114,470** na vikundi **50** vya Watu wenye Ulemavu kiasi cha **shilingi 122, 000,000.**

Naye Afisa Maendeleo ya Jamii Halmasahuri ya Wilaya ya Uyui Amoniche Mtweve amesema wamekopesha mikopo ya asilimia 10 kwa Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu.

Kikundi cha **Tunaweza** toka Kijiji cha Ilolangulu ni miongoni mwa vikundi vya Wanawake vilivyonufaika na Mikpo ya asilimia kumi ya mapato ya ndani. Kikundi hiki kimepata mkopo awamu mbili, awamu ya kwanza walikopeshwa **shilingi 5,000,000** na awamu ya pili **shilingi 5,000,000.**

Akitoa maelezo ya mafanikio ya kikundi, Mwenyekiti wa Kikundi cha Tunaweza Bi. Joha Omary Mtalima amesema kwamba, wamepata mkopo toka Halmashauri kwa ajili ya kufuga kuku chotara na kuku wa kienyeji. Katika ufugaji huo wa kuku wanaweza kupata fedha baada ya kuuza kuku na mayai na hivyo kupata mahitaji ya nyumbani, chakula na mahitaji ya shule kwa watoto wao.

Aidha, Mwenyekiti alisema kuwa baada ya kuuza kuku hao fedha nyingine watanunua vifaranga vingine kwa ajili ya kuendelea na Mradi wao.



**Mradi wa kuku kikundi cha Tunaweza**



**Wanachama wa kikundi cha Tunaweza**



**Kikundi cha Vijana (Mzambarauni ngozi) wanufaika wa mkopo asilimia kumi**



**Kikundi cha Vijana (Bodaboda Goweko) wanufaika mkopo wa asilimia kumi**



**Kikundi cha Vijana (Useremala Group) kilichpo kata ya Tura**

Jumla ya **Shilingi 8,237,000,000.00** zimetumika katika Utekelezaji wa Miradi ya mbalimbali ya Afya ikiwa ni, ujenzi wa zahanati **17**, vituo vya Afya **5** ambayo imepelekea kuongezeka kwa vituo vya kutolea huduma za Afya kutoka vituo **53** hadi **75** pamoja na ununuzi wa vifaa tiba na upatikanaji wa magari mapya **3** ya wagonjwa na **1** la usimamizi shirikishi. Hospitali ya Wilaya imeongeza huduma za macho, meno, mionzi, upasuaji, ''mortuary'' na **VVU/UKIMWI**. Aidha, Kiwango cha upatikanaji wa dawa, vitendanishi vya maabara na vifaa tiba umeongezeka kutoka asilimia **75** hadi kufikia asilimia **90**.



**Baadhi ya majengo kituo cha Afya Ilolangulu**

Jumla ya shilingi **22,709,424,300.00** zimetumika kutekeleza miradi **15** ya Maji ambapo kiwango cha upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama kimeongezeka kutoka asilimia **52** Mwaka 2021 hadi kufikia asilimia **67** kwa Mwaka 2025.




**WAKAZI WA KIJIJI CHA NYAMPINDI KATA YA KIZENGI WANUFAIKA NA MRADI WA MAJI SAFI**




**WAKALA WA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA VIJIJINI WILAYA YA UYUI (RUWASA)**







**JENGO LA OFISI YA CBWOS KIJIJI CHA SONGAMBELE KATA YA MIYENZE**



**MRADI WA BWAWA LA MAJI KIJIJI CHA KIZENGI KATA YA KIZENGI**







**WANANCHI WATUMIA VYANZO VYA MAJI VILIVYOPO KATIKA MAENEO YAO KWA AJILI YA KILIMO CHA UMWAGILIAJI NA UFUGAJI**






**KUTOKA KUSHOTO NI NDUGU LUBASHA MAKOBA MWENYEKITI WA CCM WILAYA YA UYUI**

**ALIYESIMAMA KATIKATI NI NDUGU SAID NKUMBA MWENYEKITI WA CCM MKOA WA TABORA**

**KUTOKA KULIA NI MHE. MOHAMED MTULYAKWAKU MKUU WA WILAYA YA UYUI**




**KUTOKA KUSHOTO NI**

**MHE. MOHAMED MTULYAKWAKU**

**MKUU WA WILAYA YA UYUI**

**WAPILI KUTOKA KUSHOTO NI**

**NDUGU LUBASHA MAKOBA**

**MWENYEKITI WA CCM WILAYA YA UYUI**

**WAPILI KUTOKA KULIA NI BI. LEOKADIA HUMERA MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA UYUI**

**KUTOKA KULIA NI NDUGU HABIBA MAARIFA MWENYEKITI WA JUMUIYA YA WANAWAKE WA CCM WILAYA YA UYUI**

# ASANTE SANA MAMA SAMIA




# OKTOBA TUNATIKI